



Tovuti: [www.nsimbodc.go.tz](http://www.nsimbodc.go.tz)

# Nsimbo Wiki hii....

Jarida la Wiki la Halmashauri

TOLEO NAMBA 02

NOVEMBA 18, 2018

## Wafanyabiashara wakwepa ushuru wa mazao Nsimbo kudhibitiwa,

- ⇒ *Ni mkakati wa Halmashauri kudhibiti Mapato,*
- ⇒ *Wakulima sasa kusajiliwa ,kupewa vitambulisho,*
- ⇒ *Lengo ni kutofautisha Wakulima na Wafanyabiashara wa Mazao.*



### Habari zilizomo....

- ◆ *Kamati ya Lishe Nsimbo yapatiwa mafunzo...uk 4*
- ◆ *Wananchi watakiwa kubadili Mtizamo na kuwekeza katika uwezo wa watu kufikiri...Uk..5*

Pichani: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mh.Raphael Kalinga akifungua mafunzo kwa Kamati ya Lishe Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo yaliyotolewa Novemba 12 katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.Picha na :*(Mpiga picha wetu)*

## 677, kuhitimu kidato cha Nne Nsimbo.....Uk..3

Jarida Mtandao la kila Wiki la Nsimbo Wiki Hii limeandaliwa na Kitengo cha Teknolojia ya Habari,Mawasiliano na Uhusiano

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Wasiliana nasi kupitia Barua pepe [.info@nsimbodc.go.tz](mailto:info@nsimbodc.go.tz), Tembelea tovuti yetu [www.nsimbodc.go.tz](http://www.nsimbodc.go.tz).

## Wafanya biashara wakwepa ushuru mazao kudhibitiwa .

**Na:John Mganga**

Tabia ya baadhi ya Wafanya biashara wa mazao wasio waaminifu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kutumia kisingizio cha Msamaha wa ushuru chini ya tani moja kwa wakulima ,kupitisha mazao kidogo kidogo magetini kwa kujifanya ni wakulima sasa imepatiwa mwarobaini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Mohamed Ramadhani ameeleza kuwa katika maeneo mengi Nchini baadhi ya wafanyabiashara wa mazao wasio waaminifu wamekuwa wakitumia mbinu ya kupitisha mazao magetini chini tani moja kwa kuwa kufanya hivyo kunawafanya wao kutotozwa

ushuru kwa kuwa mazao wanayokuwa wamebeba ni chini ya tani moja jambo linalowafanya kunufaika na Msamaha wa ushuru wa mazao chini ya tani moja kwa wakulima kinyume na utaratibu.

Kutokana na kukithiri kwa tabia hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wiki chache baada ya kuwasili Nsimbo tangu kuteuliwa aliagiza kuandaliwe utaratibu utakaoweze wakulima kupatiwa vitambulisho ili kudhibiti tabia ya Wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia mgongo wa msamaha wa ushuru wa mazao ya kilimo chini ya tani moja kutorosha mazao.

Hatua ya kusajili wakulima na kuwapatia vitambulisho Nsimbo kama alivyopendekeza Mkurugenzi Mo-

hamed inafuatia kuwepo kwa changamaoto ya utoroshwaji wa mazao uanofanywa na baadhi wafanyabiashara wa mazao wasio waaminifu jambo ambalo limekuwa likiathiri mapato ya Halmashauri.

Tayari utaratibu wa kusajili wakulima na kuwapatia vitambulisho umeanza kutekelezwa kwa umakini kwa kuwabaini wakulima ambapo mpaka sasa baadhi ya wakulima wamekwishapatiwa vitambulisho vitakavyowatofautisha na Wafanyabiashara wa mazao magetini.

Novemba 9, 2018 Mkurugenzi Mohamed alizungumza na wakulima wa Kata ya Kanoge katika sherehe za Uzinduzi wa Msimu wa Kilimo 2018, ambapo pamoja na mambo mengine aliwataka wakulima kujisajili kama ulivyo utaratibu ili waweze kupatiwa Vitambulisho.

Alisema kuwa Vitambulisho kwa wakulima Nsimbo vitarahisisha Halmashauri kuwatambua wakulima ndani ya Halmashauri jambo litakalosaidia kurahisisha utoaji wa huduma kwa wakulima ndani ya Halmashauri hiyo.

Alisisitiza kuwa msamaha wa Ushuru wa mazao chiniya tani moja unawahusu wakulima peke



Pichani:Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Mohamed Ramadhani Novemba9,alipozungumza wakati wa Uzinduzi wa Msimu wa Kilimo 2018 na wakulima wa Kata ya Kanoge katika eneola Kanoge Sokoni.P(icha na John Mganga)

## Wanafunzi 677,kuhitimu kidato cha Nne Nsimbo.



*Pichani:Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Katumba Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wakitoka masomoni kuelekea majumbani mwao baada ya kumaliza muda wa Masomo (Picha na :John Mganga)*

**Na:John Mganga**

*Jumla ya Wanafunzi 677 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wanatarajia kuhitimu Elimu ya kidato cha nne Novemba 23 kwa mwaka huu 2018.*

*Afisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mwl.Juma Saidi Mmaraba ameliambia Nsimbo Wiki hii kuwa Wanafunzi hao walioanza kufanya mtihani wao Novemba 5,2018 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo watamaliza Tarehe 22 Novemba 2018.*

*Akifafanua zaidi Mwalimu*

*Mmaraba amesema Wanafunzi hao wanaoendelea na mitihani ya kuhitimu elimu ya kidato cha nne katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kati yao wavulana ni 391 na wasichana ni 281.*

*Amesema kuwa mtihani huo wa taifa wa kuhitimu kidato cha nne unaendelea vema na mpaka sasa hakuna taarifa zozote za uvunjifu wa kanuni na taratibu za chumba cha mtihani zilizoripotiwa kutokea katika shule za Sekondari za Nsimbo.*

*Akizungumzia kuhusu mtihani wa kidato cha nne wa mwaka Jana 2017 Mwalimu Mmaraba amesema Wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne walikuwa 544 kati yao Wasichana 204,na Wavula-*

*na 340 sawa na asilimia 98.*

*Amesema kuwa Idadi ya wahitimu wa Kidato cha nne kwa mwaka huu 2018 imeongezeka kutoka 544 mwaka Jana na kufikia 677 kwa mwaka huu 2018 ambapo ongezeko la wahitimu wa kike wa kidato cha nne umeongezeka kutoka idadi ya Wasichana 204 mwaka 2017 hadi 286 mwaka huu 2018.*

## ***Kamati ya Lishe yapatiwa Mafunzo Maandalizi Mpango na Bajeti 2019/2020***

***Na:John Mganga***

*Kamati ya Lishe ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Novemba 12, 2018 imeptiwa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uelewa maafisa lishe kuhusu vipaumbele katika kuandaa mpango na bajeti ya Lishe kwa Meaka ujao wa fedha 2019/2020.*

*Mafunzo hayo ya siku moja kuhusu Mpango na Bajeti ya Lishe 2019/2020 yanayotolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na PANITA, na Shirika la Health Promotion yanafanyika Nchi nzima kwa lengo la kuwajengea uelewa Maafisa Lishe wa Halmashauri uelewa pamoja na kuwapitisha katika vipaumbele vya masuala muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa katika Mpango na Bajeti ya Lishe katika Halmashauri.*

*Akizungumza na Washiriki wa Mafunzo ya Mpango na Bajeti ya Masuala ya Lishe Mmoja wa wakufunzi kutoka Tmisemi amesema ni muhimu Halmashauri zikatambua umuhimu wa kutenga Bajeti ya kutosha ili kuwawezesha maafisa Lishe kote Nchini kutekeleza majukumu yao muhimu ili kunusuru Watoto na tatizo la utapiamlo.*

*Mkufunzi huyo kutoka TAMISEMI amesema ni muhimu kuwawezesha maafisa lishe ndani ya Halmashauri kutekeleza majukumu yao vizuri kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kwa sehemu kubwa kuondokana na tatizo la Udumavu wa akili utokanao na lishe duni jambo linalopeleka kuzalisha wataalamu wenye upeo mdogo wa kufikiri.*

*Amesema kuwa kutokana na kutotengewa bajeti ya kutosha maafisa Lishe katika Halmashauri kutekeleza vema majukumu yao*

*ya utoaji elimu kuhusu lishe kwa jamii ndiko kumesababisha matatizo mengi katika jamii ikiwemo kushuka kwa kiwango cha ufaulu kutokana na watoto hao kuwa na udumavu wa akili.*

*Mkufuni huyo amesema ili Jamii iweze kujenga kizazi imara chenye upeo mpana wa kufikiri ni vema Halmashauri zote Nchini zikatenga bajeti ya kutosha kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kwa sehemu kubwa kuondokana na aibu na fedheha zitokanazo na kutowekeza katika Lishe jambo linalopeleka matatizo mengi ndani ya Jamii.*

*Naye afisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Marcus Nazi amesema elimu ndogo kuhusu lishe katika mashule mengi umekuwa sababu ya watoto hao kutokuwa na ufaulu mzur kutokana na wazazi na walezi kukosa elimu ya Lishe.*

*Nazi amesema ni muhimu katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Lishe kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukajikita zaidi katika utoaji elimu mashuleni juu ya namna bora ya kuwaandaliwa watoto lishe ili kuwanusuru na tatizo kubwa la udumavu wa akili.*

*Kwa Upande wake Afisa Lishe Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bi.Tumsume Mwafumbila amesema licha ya changamoto ya uhaba wa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imefanikiwa kutoa elimu kwa Jamii kuhusu masuala ya Lishe ,pamoja na utoaji matone ya Vitamini kwa watoto wadogo kuanzia umri wa 0-5.*



*Pichani:Afisa Lishe Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bi.Tumsume Mwafumbila (aliyesimama)akitoa maelezo kuhusu Hali ya lishe ndani ya Halmashauri.(Picha na Mpiga picha wetu)*

## **Wananchi, Serikali yatakiwa kubadili mtizamo, na kuwekeza katika uwezo wa watu kufikiri.**

Ili kuwa na kizazi chenye watu wenye upeo mkubwa wa kufikiri Nchini Wananchi wametakiwa kubadili mtizamo na kuwekeza katika Lishe ili kujenga jamii yenye watu wenye upeo mpana wa kufikiri, Afisa Mipango Taakwimu na ufuatiliaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Ferdinand Filimbi ameeleza.

Filimbi ameyasema hayo Novemba 12,2018 akizungumza wakati wa Mafunzo kwa kamati ya Lishe yaliyotolewa katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri yanayohusu Mpango na Bajeti ya Lishe kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Afisa Mipango huyo ameeleza kuwa matatizo mengi yanayotokea ndani ya Jamii hapa Nchini kwa sehemu kubwa yametokana na

kosa lililofanyika tangu mwanzo la kushindwa kuwekeza kikamilifu katika Lishe kwa watoto jambo ambalo limepelekea kuleta wataalamu wenye upeo na uwezo mdogo wa kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya kijamii kutokana na athari za udumavu wa akili utokanao na utapiamlo.

Amesema ili Jamii ibadilike ni muhimu Serikali ikaweka kipaumbele katika kuwekeza kwenye eneo la elimu ya Lishe kwa jamii ili kuepuka kutengeneza kizazi chenye upeo mdogo wa kufikiri jambo linalosababisha kushamiri kwa matatizo mengi katika Jamii.

Filimbi amesema endapo Serikali itaweka Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwawezesha maafisa lishe kutoa elimu ya kutosha na Jamii ikatoa muktiko kwa kutumia vema elimu ya Lishe, itasaidia kwa kiasi kikubwa

kuondokana na tatizo la udumavu wa akili kwa watoto wadogo.

Aidha amesema kuwa Halmashauri kwa Mwaka ujao wa fedha 2019/2020 itahakikisha kuwa inaliangalia suala la lishe kwa mtizamo mpana ili kuweza kuwajengea uwezo maafisa lishe ndani ya Halmashauri na kuwatengea bajeti ya kutosa ili waweze kufikia malengo yao katika mpango kazi wao wa utoaji wa elimu kwa Jamii ili kuokoa Jamii kutoathiriwa na tatizo la utapiamlo.

Filimbi ametoa wito kwa Serikali hususani ofisi ya Rais TAMISEMI Kuhakikisha kuwa inatizama upya kada ya Maafisa lishe na kutoa muongozo utakaowawezesha kujitambua kuwa wapo katika Idara ya afya ama Kilimo.

Amesema kufanya hivyo kutawajengea Maafisa Lishe wa Halmashauri ujasiri wa kutekeleza majukumu yao ya utoaji wa elimu kwa kujiamini jambo litakalochangia kufikiwa malengo mahsusi ya kutekeleza adhema ya serikali ya kuondoa tatizo la dumavu wa akili kwa watoto tatizo litokanalo na utapiamlo.

Mafunzo hayo ya siku moja yanayohusu Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Lishe kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yamefanyika kwa siku moja ambapo kamati ya Lishe Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imepitishwa katika vipaumbele vina vyotakiwa wakati wa maandalizi ya Baeti ya Lishe kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020.

Kwa upande wao washiriki wa mafunzo hayo wamesema mafunzo hayo yamefanyika kwa wakati muafaka na watazingatia waliyofundishwa kwa utekelezaji.



Pichani: Afisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji (W) Bw.Ferdinand Filimbi akichangia mada wakati wa Mafunzo kwa Kamati ya Lishe yaliyotolewa Novemba 12 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri (Picha na: John Mganga)